

Bwana aliposema kuwa yeye ni “Mungu wa miungu” alikuwa na maana gani?..je! yeye ni Mungu wa sanamu?

JIBU: Tukisoma Kumbukumbu 10:17 inasema...

“Kwa maana Bwana, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa mabwana, Mungu mkuu, mwenye kuogofya, asiyependelea nyuso za watu, wala hakubali rushwa”.

Hapa tunaona Mungu anajitambisha yeye kama **“Mungu wa miungu”** sasa swali hawa miungu ni wakina nani?. Bwana Yesu alisema mahali fulani katika kitabu cha Yohana,..

Yohana 10:33 “Wayahudi wakamjibu, Kwa ajili ya kazi njema hatukupigi kwa mawe; bali kwa kukufuru, na kwa sababu wewe uliye mwanadamu wajifanya mwenyewe u Mungu.

34 Yesu akawajibu, Je! Haikuandikwa katika torati yenu ya kwamba, Mimi nimesema, Ndinyi miungu?

35 Ikiwa aliwaita miungu wale waliojiliwa na neno la Mungu; (na maandiko hayawezi kutanguka);

36 je! Yeye ambaye Baba alimtakasa, akamtuma ulimwenguni, ninyi mniamwambia, Unakufuru; kwa sababu nalisema, Mimi ni Mwana wa Mungu?”

Bwana aliposema kuwa yeye ni “Mungu wa miungu” alikuwa na maana gani?..je! yeye ni Mungu wa sanamu?

Kwahiyo unaona hapo miungu inayozungumziwa hapo ni WATOTO WA MUNGU, (yaani sisi tuliomwamini yeye na kuoshwa kwa damu yake) inadhaniwa na wengi kuwa miungu iliyozungumziwa pale ni “SANAMU” LA! sivyo. Mungu hawezi akawa ni Mungu wa sanamu. Sanamu hata siku moja haziwezi zikampa Mungu utukufu, Na tunajua tabia za miungu ni lazima zifanane na Mungu, Hivyo basi kazi zile zile Mungu anazozifanya lazima na miungu izifanye, kwa mfano Mungu alitumia NENO lake kuumba na kufanya kila kitu na sisi vivyo hivyo kwa NENO lake tunaweza tukafanya kazi za Mungu vile vile kama yeye. Lakini tusipoweza kufanya hivyo inamaana sisi sio miungu kwasababu hatufanani na yeye. ni sawasawa tu na alivyojiita yeye ni MFALME wa wafalme, au BWANA wa mabwana.

Kwahiyo ili sisi tuwe miungu lazima tuwe ni WATOTO WA MUNGU wenyе tabia kama za kwake nazo ni: Upendo, Imani, Haki, Utakatifu, utu wema, kiasi n.k Wagalatia 5:22 hivyo tuzidi kutia bidii katika kumjua yeye ili tustahili kuitwa miungu.

Maelezo haya unaweza kuyapata kwa njia ya video mwisho wa somo hili

**Ubarikiwe sana. jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa
>> [WHATSAPP](#)**

Bwana aliposema kuwa yeye ni “Mungu wa miungu” alikuwa na maana gani?..je! yeye ni Mungu wa sanamu?

[embedyt] <https://www.youtube.com/watch?v=Jqkm6O2IdUQ> [/embedyt]

Mada zinazoendana:

**BWANA YESU ALIKUWA ANAONYESHA KUWA MUNGU NI
MUNGU MWENYE AKILI TIMAMU.**

**JE! MUNGU ANAWEZA KULETA MAJIBU KUPITIA NGUVU ZA
GIZA KAMA ALIVYOFANYA KWA MFALME SAULI?**

ACHENI MJUE YA KUWA MIMI NI MUNGU.

UWEZA WA MUNGU UNAONEKANA WAPI?

Rudi Nyumbani

Share on:

WhatsApp